**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 1 No. 2 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i2.393


# Ujitokezaji wa Viarudhi vya Kifonolojia katika Kihaya: Uchunguzi Kifani wa Toni katika Lahaja ya Kihamba

**Editha Adolph**
*Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Tanzania*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2023-10-23*
*Rekebishwa: 2023-11-10*
*Kubalika: 2023-12-30*
*Chapishwa: 2023-12-31*

***Maneno Muhimu***
Fonolojia
Kihamba
Toni
Viarudhi

***Jinsi ya Kurejelea Makala:***
Adolph, E., (2023). Ujitokezaji wa Viarudhi vya Kifonolojia katika Kihaya: Uchunguzi Kifani wa Toni katika Lahaja ya Kihamba. *Journal of Kiswahili and Other African Languages, 1*(2), 29-42.

*Copyright © 2023 The Author*
CC BY

**Ikisiri**
Fonolojia ni taaluma iliyosheheni viarudhi au vipambasauti kama ambavyo wataalamu wengine huviita. Miongoni mwake ni toni, lafudhi, mkazo, nguvumsikiko, usilabi, kiimbo, unguvunguvu, kidatu na wakaa. Viarudhi hivi hupatikana takribani katika kila lugha ingawaje baadhi ya lugha huwa navyo vichache na kukosa baadhi. Toni ni miongoni mwa viarudhi vinavyojitokeza katika Kihaya. Makala hii inachunguza jinsi kiarudhi hiki kinavyojitokeza katika Kihaya hususan lahaja ya Kihamba na namna ambavyo huathiri maana ya msamiati sambamba na kubadili kategoria katika lahaja hiyo. Lahaja ya Kihamba ni miongoni mwa lahaja za Kihaya. Lahaja nyinginezo za lugha hii ni: Kinyaihangiro, Kinyambo na Kiziba. Data ya makala hii imekusanywa uwandani kwa kushuhudia mazungumzo mbalimbali ya wazungumzaji wa lahaja ya Kihamba katika nyakati tofautitofauti na sehemu mbalimbali, pia mbinu ya usaili kutoka kwa wazungumzaji wa lahaja hii ilitumika. Ulifanyika pia uchambuzi wa matini mbalimbali kutoka maktabani mathalani, kamusi, majarida, tasinifu, tafiti na nyaraka mbalimbali zinazohusiana na mada inayoshughulikiwa katika makala hii. Kwa kutumia mbinu ya usaili, nomino na vitenzi mbalimbali viliandaliwa kwa Kiswahili na watoa taarifa walihitajika kuvitamka kwa Kihaya hususani Kihamba huku mtafiti akirekodi na kualamisha toni katika nomino na vitenzi hivyo. Data imechanganuliwa kwa kutumia mkabala wa maelezo. Nadharia iliyotumika kuchanganua data ya makala hii ni Nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru iliyoasisiwa na Goldsmith (1976). Matokeo ya makala hii yanaonesha kuwa toni hujitokeza katika Kihaya hususani lahaja ya Kihamba. Imebainika pia kuwa toni hizi zimesheheni uamilifu wa kubadili maana na kategoria za msamiati kutokana na tofauti za kimatamshi zinazosababishwa na matumizi ya toni ya juu au ya chini katika msamiati wenye kufanana kiothografia. Aidha, matokeo yanaonesha kuwa si kila kitenzi au nomino hutamkwa kwa namna tofauti kutokana na kutokubali kupokea toni juu J (kuanzia sasa) na wakati huohuo toni chini C (kuanzia sasa). Aidha, makala hii imetoa ufafanuzi na kuonesha uamilifu wa toni katika lahaja ya Kihamba na hivyo kuwapa mwanga

wanaisimu juu ya kiarudhi hiki cha kifonolojia. Inapendekezwa kuwa viarudhi vingine mathalani lafudhi, mkazo, nguvumsikiko, usilabi, kiimbo, unguvunguvu, kidatu na wakaa vifanyiwe uchunguzi katika Kihaya na lugha nyinginezo. Pia lichunguzwe suala la ujitokezaji wa toni katika aina nyingine za maneno katika lugha hii tofauti na nomino na vitenzi. Kwa mfano, vielezi, vivumishi, vihisishi na kadhalika. Aidha, tafiti fuatizi zaweza kuangazia matumizi ya toni katika lugha za Kiafrika.

**Utangulizi**

Lugha ya Kihaya ni miongoni mwa lugha zilizo na kiarudhi au kipambasauti cha toni. Viarudhi au vipambasauti ni vipengele ambavyo huhusishwa na vitamkwa vinavyojenga maneno katika utamkaji wake. Viarudhi au vipambasauti hivyo hubainika tu vinapokuwa vimehusishwa na vitamkwa, kwamba haviwezi kusimama peke yake bila kuhusishwa na vitamkwa vilivyo dhahiri. Tunapozungumzia toni tunamaanisha kiwango pambanuzi cha kidatu cha silabi katika neno au sentensi kiwezacho kubadilisha maana ya neno au sentensi husika kisemantiki na hata kisarufi. Toni huweza kujitokeza katika silabi, neno na katika sentensi. Kwa hivyo, ujuzi wa kiarudhi cha toni ni muhimu hasa katika kupambanua maana katika baadhi ya lugha za Kiafrika. Massamba (2016) anaeleza kuwa toni ni sifa inayowakilisha kiwango pambanuzi cha kidatu cha silabi katika neno au sentensi na ambayo huweza kubadili maana ya neno au sentensi hiyo kisemantiki au kisarufi. Toni hutumika kwa kiwango kikubwa katika lugha za Kibantu. Suala hili linaungwa mkono na Kihore na wenzie (2008) wanaoeleza kuwa ni muhimu kuzingatia kwamba lugha nyingi za Kibantu hutumia zaidi toni kuliko mkazo.

**Matumizi ya Toni katika Lugha Mbalimbali**

Imeelezwa awali (taz. § 1.0) kuwa toni hutumika kwa kiwango kikubwa katika lugha za Kibantu. Sambamba na hilo, kiarudhi hiki kina matumizi mengi katika lugha kama inavyofafanuliwa na wanazuoni kadhaa: (Pike, 1948; Carte, 1973; Byarushengo, 1975; Byarushengo, Larry na Sarah, 1976; Hyman na Byarushengo, 1984; Kisseberth, 1984; Bird 1999; Kisseberth na David 2003; Odden, 2005; na Massamba, 2011). Mtaalamu mwingine aliyeshughulikia toni ni Leben (1978). Leben alichunguza toni katika lugha ya Kimende. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa toni katika Kimende hubadilikabadilika na hazina mpangilio mahususi katika msamiati wake. Mifano ifuatayo inathibitisha hilo:

| **Kimende** | **Kiswahili** |
|---|---|
| Fàndé | pamba |
| bɛlɛ | suruali |
| pɛlɛ | nyumba |
| ngílà | mbwa |

**Chanzo**: Leben (1978)

Mifano iliyotolewa hapo juu inadhihirisha kuwa toni katika Kimende si tabirifu kwani kila neno lina mpangilio tofauti na neno jingine. Sambamba na wataalamu hao, Muzale (2006) katika utafiti wake kuhusu matumizi ya toni katika Kihaya anadhihirisha kuwa lugha ya Kihaya ina aina tatu za toni.

Mosi, toni chini (L[1]), pili, toni juu (H[2]), tatu, toni mshuko (HL[3]). Muzale (2006) Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa katika lugha ya Kihaya, toni hizi hutokea kwa namna/mitindo tofautitofauti, kama ilivyooneshwa katika mifano ifuatayo:

| **Toni Chini** | **Msamiati wa Kihaya** | **Maana katika Kiswahili** |
|---|---|---|
| L-L | ku-sa | kusaga |
| L-L.L | ku-bara | kuhesabu |
| L-L.L.L | ku-shereka | kuficha |
| | | |
| L-L.L.L.L.L | ku-shoholerana | kutokezea upande wa pili |
| L-L.L.L.L.L | e-bishankulima | takataka |

**Chanzo:** Muzale (2006)

| **Toni Juu (H) na Mshuko (HL)** | **Msamiati wa Kihaya** | **Maana katika Kiswahili** |
|---|---|---|
| H-L | kú-ba | kuwa |
| L-H.L.L | ku-kórora | kukohoa |
| L-L.H.L.L.L | a-karángaishuko | hali ya kutokuwa makini |
| L-L.H.L.L.L | e-kiráraigoro | kumbikumbi wa jioni |
| L-L.L.L.H.L | a-kakomamúti | gogota |

**Chanzo:** Muzale (2006)

Mifano iliyotolewa hapo juu inadhihirisha wazi kuwa toni hujitokeza katika lugha ya Kihaya kama alivyobainisha Muzale (2006). Utafiti huu ni muhimu kwani umemwongoza mtafiti wa makala hii kung'amua kuwa kiarudhi hiki cha toni hujitokeza katika lugha ya Kihaya. Hata hivyo, utafiti wa Muzale (2006) umeelezea kwa ufupi sana juu ya toni katika lugha ya Kihaya kutokana na sababu kuwa dhana hii ilijitokeza katika *Ikaning'ambo ya Oruhaya* (Kamusi ya Kihaya) kwa ufupi sana. Lengo la kamusi hii ni kwa ajili ya kuzifafanua, kuziwekea kumbukumbu na kuzidumisha lugha zetu za Tanzania. Lengo likiwa hasa kwa ajili ya makundi mawili. Moja, likiwa kundi la wazungumzaji wa Kihaya ambao kwao hii ni hazina ya msamiati na maneno ya lugha yao pamoja na visawe vyake katika Kiswahili na Kiingereza. Pili, ni kundi la watafiti katika uga wa isimu ili waweze kupata data ya kuchambua, kufafanua na kulinganisha lugha. Hivyo, si lengo la kamusi hii kuonesha toni na dhima zake katika lugha ya Kihaya isipokuwa kipengele hicho kimejitokeza kwa kiasi kidogo sana ili kutoa uelewa kwa msamiati utakaokuwa umetumia kiarudhi hiki cha kifonolojia (toni) ndani ya kamusi hiyo. Aidha, Muzale (2006) ameonesha ujitokezaji wa toni katika neno mojamoja na siyo maneno mawili yenye kufanana kiothografia na kutofautishwa na toni katika utamkwaji wake. Pia hakuelezea dhima za toni katika maneno aliyoyabainisha. Tofauti na utafiti huo, mtafiti wa makala hii anatoa ufafanuzi wa kina juu ya ujitokezaji wa toni katika Kihaya husuan lahaja ya Kihamba ikijiegemeza katika nomino na vitenzi akionesha namna msamiati uleule unavyotamkwa kwa namna

[1] Alama aliyoitumia kwa toni chini.
[2] Alama aliyoitumia kwa toni juu.
[3] Alama aliyoitumia kwa toni mshuko. Katika makala hii mtafiti anatumia alama 'J' kuonesha toni ya juu na 'C' kuonesha toni ya chini tofauti na zile za Muzale.

Vol. 1 No. 2 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i2.393


tofauti kutokana na aina ya toni husika sambamba na kuonesha maana ya msamiati na uamilifu wa toni hizo katika msamiati husika.

Kwa upande wake Massamba (2011), amechunguza ujitokezaji wa toni katika lugha ya Kihaya na Ci-Ruuri. Utafiti wake unaonesha kuwa mojawapo ya sifa za toni katika lugha hizi ni kuhama. Ametoa mifano ifutayo ili kuthibitisha madai hayo:

(a)

| **Kihaya** | **Kiswahili** |
|---|---|
| Omúti | mti |
| Obugólo | ugolo |

(b)

| **Kihaya** | **Kiswahili** |
|---|---|
| Omutí gwange | mti wangu |
| Obugoló bwange | ugolo wangu |

(c)

| **Ci-Ruuri** | **Kiswahili** |
|---|---|
| Okutéma | kukata |
| Okukáma | kukama |

(c)

| **Ci-Ruuri** | **Kiswahili** |
|---|---|
| Okuteméra | kukatia |
| Okukamíra | kukamia |

**Chanzo**: Massamba 2011

Kutokana na mifano hiyo hapo juu, Massamba (2011) anasema kuwa irabu ambazo zilikuwa zimebeba toni juu sasa hazina toni juu tena. Badala yake toni hiyo imehamia kwenye silabi zinazofuata. Anaendelea kusema kwamba sifa ya toni haiwezi kuwa sehemu ya irabu inayohusishwa nayo vinginevyo isingeweza kuhama, ikatoka kwenye irabu hiyo na kwenda kwenye irabu ya silabi nyingine. Hivyo, Massamba (2011) anaunga mkono hoja ya kwamba moja ya sifa ya toni ni kuhama kutoka kwenye irabu husika na kwenda kwenye irabu ya silabi nyingine. Aidha, anaunga mkono hoja ya kwamba sifa ya toni haiwezi kuwa sehemu ya irabu inayohusishwa nayo na ndiyo maana huweza kuhama ikatoka kwenye irabu hiyo na kwenda kwenye irabu ya silabi nyingine. Hoja hii inaungwa mkono na Kindole (2012) anayeeleza kuwa asilimia 97 ya lugha za Kibantu zina toni na mojawapo ya sifa ya kuvutia ya lugha za Kibantu ni sifa ya uhamaji wa toni hizo. Kindole amechunguza ruwaza ya toni katika vitenzi vya lugha ya Kihehe na kuthibitisha kuwa, mosi, utokeaji wa toni katika vitenzi vya lugha hii hutegemea idadi ya silabi za shina la kitenzi, pili, kiinitoni katika vitenzi vyote kinaangukia katika silabi ya mwisho kasoro moja, tatu, kiinitoni kinahusishwa na toni juu. Tafiti hizi ni faafu katika makala yetu kwani zinatuonesha sifa za toni, ruwaza na ujitokezaji wa toni katika lugha za Kibantu mathalani lugha ya Kihaya, Ci-Ruuri na Kihehe. Mtafiti wa makala hii miongoni mwa mambo anayoyachunguza ni kuhusiana na toni katika lugha ya Kihaya suala lililoshughulikiwa na Massamba. Hata hivyo, mtafiti wa sasa anachunguza namna toni zinavyoathiri maana ya msamiati katika lugha ya Kihaya na si uhamaji wa toni kama matokeo ya utafiti wa Massamba (2011) yanavyoonesha. Aidha, makala hii haishughulikii ruwaza ya toni kama ilivyo kwa Kindole (2012). Naye Downing (2013) amechunguza dhana ya toni katika lugha ya Kitsonga. Matokeo ya utafiti wake yanabainisha kuwa toni katika lugha ya Kitsonga huhusika katika kuonesha uhusiano wa fonolojia na sintaksia. France na Kahigi (2021) nao wanasema kuwa urefushaji wa irabu katika Kinyambo (lahaja ya Kihaya) unaambatana na mabadiliko ya toni na kuwa toni ya juu katika baadhi ya maneno

ya Kinyambo. Halikadhalika, Mramba (2020), amechunguza ruwaza za toni katika vitenzi visoukomo changamani vya Kirombo. Miongoni mwa masuala aliyoyabaini ni kwamba toni katika Kirombo hubadili kategoria ya maneno kama inavyoonekana katika mfano hapa chini:

| Msamiati wa Kirombo | Maana katika Kiswahili | Kategoria |
|---|---|---|
| i-kerésa | gereza | (N) |
| i-kéresa | chonga kitu | (T) |
| sháa | nje | (N) |
| shaá | beza/kataa | (T) |
| i-sháa | kuja | (T) |
| i-shaá | ukucha mkubwa | (N) |
| káa | kaa la moto | (N) |
| i-kàa | kukaa/kuishi mahala fulani | (T) |

**Chanzo**: Mramba (2020)

Kutokana na utafiti wa Mramba (2020), mtafiti wa makala hii amebaini kuwa pamoja na toni kubadili kategoria ya maneno katika Kihaya, suala hili hujitokeza pia katika lugha nyinginezo kama vile lugha ya Kirombo. Tofauti na utafiti wa Mramba (2020) ulioshughulikia ruwaza za toni katika vitenzi visoukomo changamani vya Kirombo, makala hii inashughulikia ujitokezaji wa toni katika Kihaya hususani lahaja ya Kihamba sambamba na uamilifu wa toni hizo.

**Lugha ya Kihaya**

Kihaya ni miongoni mwa lugha za Kibantu inayozungumzwa mkoani Kagera katika maeneo ya Kaskazini-Magharibi mwa Tanzania. Lugha hii pia huitwa: Ekihaya, Luhaya pia Oluhaya. Guthrie Malcolm (1971) ameiainisha lugha hii katika kundi la E 20 na E 22 ilhali Maho (1999) ameiainisha katika kundi la JE22. Lugha hii imesheheni viarudhi vya kifonolojia kama vile: toni, lafudhi, kiimbo, wakaa, kidatu na kadhalika. Byarushengo, (1977) anabainisha lugha mbalimbali zinazohusiana na lugha ya Kihaya. Lugha hizo ni: Kinyankole, Kikinga, Kinyarwanda, Kishubi, Kizinja, Kirundi, Kiha, Kinyoro, Kiganda na Luhya. Muzale (2006) kwa upande wake, ameainisha lugha mbalimbali zinazohusiana na Kihaya mfano, Kinyambo, Kizinza, Kisubi na Kikerewa kutoka nchini Tanzania ilhali Runyoro, Rutooro na Runyankore zikiwa ni lugha za Uganda. Naye Buberwa (2015) anaongezea kwa kueleza kuwa lugha ya Kihaya kama zilivyo lugha ndogondogo nyingi nchini Tanzania, inazungumzwa katika maeneo machache ya nchi na lugha hii hutumika katika mazungumzo ya kila siku yasiyo rasmi.

**Lahaja ya Kihamba**

Kihamba ni mojawapo ya lahaja za lugha ya Kihaya. Kihamba huzungumzwa katika wilaya ya Muleba kata za Izigo, Muhutwe, Mayondwe na Kamachumu. Muzale (2006) anabainisha kuwa mbali na Kihamba, lahaja nyingine za lugha ya Kihaya ni: Kinyaihangiro (Orunyaihangiro), Kinyambo (Orunyambo), Kiyoza (Oruyoza) na Kiziba (Oruziba).

**Kiunzi cha Nadharia**

Mtafiti wa makala hii ametumia Nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru ambayo muasisi wake ni Goldsmith (1976). Goldsmith (1976) ametoa mihimili mikuu miwili kuhusiana na Nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru. Mhimili wa kwanza unahusu uchanganuzi wa vipengele vya kifonolojia. Kwamba kila kipengele kiwe na rusu yake. Kwa hiyo, katika uchanganuzi wa vipengele vya kifonolojia lazima kuwe na rusu ya vitamkwa, rusu ya toni na rusu ya kiimbotoni kama inavyooneshwa katika mifano ifuatayo:

Vol. 1 No. 2 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i2.393


**Kielelezo Na. 1**

KI + KI + KI +KI → Rusu ya vitamkwa
| | | | → Mistari ya uhusiano
**J C J C** → Rusu ya kiimbotoni

Mhimili wa pili ni kuhusiana na kupunguza sheria za kubadili sifa wakati wa kufanya uchanganuzi wa vipengele vya kifonolojia. Tuangalie mfano ufuatao kwa uelewa zaidi:

**Kielelezo Na. 2**

K I K I # # I K I > K I K + I K I
C J C J C JC J

Kielelezo Na 2 hapo juu kinaonesha kuwa irabu ya mwisho ya neno la kwanza imetoweka huku toni iliyokuwa imehusishwa na irabu hiyo ikibaki kwani toni kwa mujibu wa Nadharia ya Vipandesauti Huru si kiambajengo cha kitamkwa. Nadharia hii ni muafaka katika makala hii kwani imetuongoza katika suala zima la rusu ya vitamkwa, rusu ya toni na rusu ya kiimbotoni kama ilivyojitokeza katika kipengele cha uchambuzi wa data §[4] 4.0.

**Methodolojia**

Utafiti huu umefanyika katika mkoa wa Kagera wilaya ya Muleba kata za Izigo na Muhutwe. Maeneo haya ni muafaka kwani ndiko inakozungumzwa lahaja ya Kihamba. Ili kufikia malengo yake, mtafiti ametumia mbinu mbalimbali za utafiti katika ukusanyaji na uchambuzi wa data ya makala hii. Miongoni mwa mbinu zilizotumika ni pamoja na ushuhudiaji, usaili pamoja na uchambuzi wa matini kutoka katika chanzo cha data cha maktabani. Mikabala ya uwandani na maktabani kwa pamoja ilimwezesha mtafiti kukusanya data nyingi na kufanya majumuisho ya matokeo ya makala hii. Usaili ni mbinu ya ukusanyaji wa taarifa inayohusisha uulizaji wa maswali kwa njia ya mdomo, majadiliano, majibizano ya ana kwa ana au kwa njia ya simu. Lengo la mtafiti kutumia mbinu hii ni kukusanya taarifa na maoni kutoka kwa watafitiwa kuhusiana na suala la kiutafiti. Kwa kutumia mbinu ya usaili, nomino na vitenzi viliandaliwa kwa Kiswahili na watoa taarifa walihitajika kuvitamka kwa Kihamba huku mtafiti akirekodi na kualamisha toni katika nomino na vitenzi hivyo. Mbinu hii pia ilisaidia kupata maoni na mtazamo wa watafitiwa kuhusu ujitokezaji wa toni katika Kihaya hususan lahaja ya Kihamba na uamilifu wake. Ushuhudiaji ni mbinu inayompa mtafiti wasaa wa kuangalia na kufanya uchunguzi wa kina juu ya kile anachokitafiti. Wahusika wa mbinu hii walikuwa wazungumzaji wa lahaja ya Kihamba. Data iliyokusanywa kupitia mbinu hizi kutoka uwandani, ni ile iliyoonesha namna toni hujitokeza katika msamiati wa Kihamba na namna toni hizo zinavyoathiri maana ya msamiati wenye kufanana kiothografia kutokana na aina ya toni iliyotumika. Kwa upande wa chanzo cha data cha maktabani, mtafiti alifanya uchambuzi wa matini kwa kusoma nyaraka mbalimbali kama vile: majarida, kamusi, tasinifu na kadhalika. Kutokana na chanzo hiki cha data, mtafiti alibaini namna toni zinavyojitokeza katika lugha mbalimbali hasa lugha za Kibantu, ruwaza ya toni na kuhama kwa toni. Baada ya kuona mbinu za utafiti wetu, tuangalie kipengele cha matokeo ya utafiti.

[4] Sehemu

**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 1 No. 2 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i2.393


## Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya makala hii yanathibitisha kuwa lugha ya Kihaya imesheheni toni ambazo ni mojawapo ya viarudhi vya kifonolojia. Toni, kwa mujibu wa taarifa za watafitiwa ni kwamba, zina uwezo mkubwa wa kubadili maana ya msamiati wenye kufanana kiothografia katika lugha ya Kihaya hususan lahaja ya Kihamba. Mifano ifuatayo inaonesha namna toni zinavyojitokeza katika lahaja ya Kihamba na uamilifu wake.

### Toni katika Nomino za Kihaya

Matokeo ya makala hii yamebainisha kuwa toni hujitokeza katika nomino za Kihaya hususan lahaja ya Kihamba. Toni zinazojitokeza katika nomino hizi ni C na J. Toni hizi kwa kawaida zina uamilifu wa kubadili maana na hata kategoria ya msamiati husika japokuwa si msamiati wote utabadili kategoria yake. Suala la kubadili maana na kategoria kwa msamiati wenye kufanana kiothografia lakini ukawa na toni tofauti kama vile C na J litajadiliwa § 4.3. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Vipandesauti Huru, mtafiti amekipa kila kipengele rusu yake kama ambavyo imejitokeza katika Kielelezo No. 1 hapo juu. Tuangalie namna toni zinavyojitokeza hatika nomino za Kihamba kutokana na mifano iliyotolewa hapa chini.

| **Nomino za Kihamba** | **Maana katika Kiswahili** |
|---|---|
| ékyáí<br>J JJ | kamba ya mgomba |
| èkyàì<br>C C C | chai |
| éndá<br>J J | chawa |
| èndà<br>C C | mimba |
| énkází<br>J J J | mnyama yeyote mwenye jinsi ya kike yaani jike |
| ènkàzì<br>C C C | uvimbe unaojipandikiza kwenye mwili wa binadamu ambao mwonekano wake uko kama nundu. |

mwízí aina ya ugonjwa[5]
| |
J J

mwìzì mhamiaji yaani mtu asiye mzawa wa eneo husika.
| |
C C

Rúhángá muumbaji
| | |
J J J

rùhàngà mtaro
| | |
C C C

**Chanzo**: Data ya Uwandani, 2023.

Mifano iliyotolewa hapo juu ni uthibitisho tosha kuwa toni hujitokeza katika nomino za Kihaya hususan zile za lahaja ya Kihamba. Baada ya kuona ni kwa jinsi gani toni hujitokeza katika nomino za lahaja ya Kihamba, tuone ni kwa namna gani pia hujitokeza katika vitenzi vya lahaja hii:

**Toni Zinavyojitokeza katika Vitenzi vya Kihamba**

Kupitia mbinu ya ushuhudiaji na usaili imethibitika kuwa pamoja na toni kujitokeza katika nomino za Kihamba pia hujitokeza katika vitenzi vya lahaja hiyo kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo.

**Vitenzi vya Kihamba** **Maana katika Kiswahili**

kúsíngá kusugua
| | |
J J J

kùsìngà kufaulu
| | |
C C C

kúúná kuguna
| | |
J J J

kùùnà Hali ya kujificha kwa lengo la kusikiliza au kuangalia jambo
| | |
C C C kwa siri/kuvizia

náándíká anaandika
| | | |
J J J J

nààndìkà nimeandika
| | | |
C C C C

[5] Ugonjwa wa Kihaya unaojulikana kama *ndwala nkuru*. Ugonjwa huu hasahasa huharibu mimba au hata huyafanya maziwa ya mama kukosa virutubisho, yanakuwa majimaji.

náchwá anatema
| |
J J
nàchwà nimetema
| |
C C
nágéndá anaenda
| | |
J J J

nàgèndà naenda
| | |
C C C
náyómbéká anajenga
| | | |
J J J J
nàyòmbèkà nimejenga
| | | |
C C C C
názárá anajifungua
| | |
J J J
nàzàrà nimejifungua
| | |
C C C

**Chanzo:** Data ya Uwandani, 2023.

Matokeo ya makala hii kupitia mbinu ya ushuhudiaji na usaili, yanaonesha wazi kuwa toni zinajitokeza katika vitenzi na nomino za Kihaya hususani lahaja ya Kihamba. Imebainika pia kuwa toni hizo huwa na uamilifu kadhaa katika vitenzi na nomino za lugha hiyo. Miongoni mwa uamilifu huo ni: mosi, kubadili kategoria ya msamiati husika. Pili, kubadili maana ya msamiati. Tuangalie mifano ifuatayo kwa uelewa zaidi.

**Uamilifu wa Toni katika Kubadilisha Maana ya Msamiati wenye Kufanana Kiothografia**

Matokeo ya makala hii yanaonesha kuwa toni katika lugha ya Kihaya hususan lahaja ya Kihamba hubadili maana ya msamiati wenye kufanana kiothografia. Hii inathibitika kupitia mifano iliyotolewa ili kuthibitisha ukweli huu:

| **Toni Juu** | **Maana** | **Toni Chini** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| éká<br>\| \|<br>J J | beba mgongoni | èkà<br>\| \|<br>J J | familia |

Vol. 1 No. 2 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i2.393


| | | | |
|---|---|---|---|
| chúmbá<br>J J | pika | chùmbà<br>C C | chumba |
| kyárá<br>J J | tembea | kyàrà<br>C C | kidole |
| mbálá<br>J J | huwa nahesabu | mbàlà<br>C C | kupe |
| ndámanya<br>J | huenda, labda | ndàmanya<br>C | nitajua |
| yáyá<br>J J | mlezi wa watoto | yàyà<br>C C | Tendo la mtu kuungua |

**Chanzo:** Data ya Uwandani, 2023

Data hapo juu inaonesha msamiati unaofanana kiothografia lakini maana yake hutofautishwa na toni. Hii inathibitisha dhahiri kuwa toni katika lugha ya Kihaya hususani lahaja ya Kihamba, ina uamilifu wa kubadili maana ya msamiati wenye kufanana kiothografia.

**Uamilifu wa Toni katika Kubadilika Kategoria ya Msamiati**

Mbinu alizotumia mtafiti wa makala hii; usaili na ushuhudiaji, zimemthibitishia kuwa pamoja na toni kuwa na uamilifu wa kubadili maana ya msamiati katika lugha ya Kihaya hususan lahaja ya Kihamba, pia hubadili kategoria ya msamiati wenye kufanana kiothografia kama inavyojadiliwa hapa chini:

| Toni Juu | Kategoria | Toni Chini | Kategoria |
|---|---|---|---|
| éká<br>J J | T | èkà<br>J J | N |
| chúmbá<br>J J | T | chùmbà<br>C C | N |
| mbárá<br>J J | T | mbàrà<br>C C | N |
| yáyá<br>J J | T | yàyà<br>C C | N |

**Chanzo:** Data ya Uwandani, 2023

**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 1 No. 2 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i2.393


Data hapo juu inadhihirisha wazi kuwa japokuwa toni huwa na uamilifu wa kubadili maana ya msamiati katika lahaja ya Kihamba, pia hubadili kategoria ya msamiati wenye kufanana kiothografia.

**Nomino Zinazotamkwa kwa Namna Moja tu**

Data ya makala hii inadhihirisha wazi kuwa katika lugha ya Kihaya husuan lahaja ya Kihamba, si kila nomino hukubali C na J kama ilivyo katika § 4.1 na badala yake zipo nomino zinazotamkwa kwa namna moja tu. Katika § 4.1 tumeona kuwa nomino kadhaa hufanana kiothografia na maana yake kutofautishwa na C na J. Mifano inayotolewa hapa chini ni kinyume chake kwa maana kuwa hazipokei toni zote mbili yaani C na J kwa pamoja na badala yake hukubali aina mojawapo ya toni hizi. Mifano ifuatayo inathibitisha ukweli huu.

| **Nomino Inayokubalika** | **Nomino Isiyokubalika** | **Maana katika Kiswahili** |
|---|---|---|
| amatúnda | **amatùnda | matunda |
| J | C | |
| amázi | **amàzi | kinyesi |
| J | C | |
| empúnu | **Empùnu | nguruwe |
| J | C | |
| eyómbo | **eyòmbo | kelele |
| J | C | |
| omushóro | **omushòro | ushuru |
| J | C | |
| omúti | **omùti | mti |
| J | C | |
| obugólo | **obugòlo | ugolo |
| J | C | |
| orúfu | **orùfu | kifo |
| J | C | |

**Chanzo:** Data ya Uwandani, 2023

Mifano iliyofafanuliwa hapo juu, inathibitisha kuwa katika lahaja ya Kihamba kuna nomino zinazotamkwa kwa namna moja tu. Hii ina maana kuwa si kila nomino hukubali C na J.

**Vitenzi Vinavyotamkwa kwa Namna Moja tu**

Watafitiwa wa makala hii kupitia mbinu ya ushuhudiaji na usaili, wamethibitisha kuwa katika lugha ya Kihaya hususan lahaja ya Kihamba kuna baadhi ya vitenzi vinavyotamkwa kwa namna moja tu tofauti na ilivyojitokeza katika § 4.2. Pamoja na vitenzi mbalimbali (rejea katika § 4.2) kufanana kiothografia na kutamkwa kwa namna tofauti kutokana na kuathiriwa kwa C na J, pia vipo vighairi vyake kama vinavyodadavuliwa hapa chini:

| Kitenzi Kinachokubalika | Kitenzi Kisichokubalika | Maana katika Kiswahili |
|---|---|---|
| bóneka (J) | **bòneka (C) | onekana |
| ekigúnju (J) | **ekigùnju (C) | mnyama |
| ítoitora (J) | **ìtoitora (C) | dadavua |
| kwékenga (J) | **kwèkenga (C) | epuka jambo fulani |
| rúmika (**J**) | **rùmika (**C**) | tendo la kutoa damu kwa binadamu au mnyama |

Data ya makala yetu kupitia mbinu ya usaili na ushuhudiaji, inaonesha wazi kuwa katika lahaja ya Kihamba kuna baadhi ya vitenzi vinavyotamkwa kwa namna moja na havikubali matumizi ya C na J kwa wakati mmoja kama ilivyobainishwa katika § 4.2. Aidha, **k**atika data yetu hapo juu, msamiati wote uliowekewa nyota hauwezi kutamkwa namna hiyo katika lahaja ya Kihamba. Isipokuwa huweza kutamkwa hivyo katika lahaja nyinginezo za Kihaya. Mathalani, utamkaji huu hujitokeza katika lahaja nyingine ya Kihaya; Olunyaihangiro na siyo katika lahaja ya Kihamba.

**Hitimisho**

Ni dhahiri kuwa kiarudhi cha kifonolojia; toni (C na J), hujitokeza katika lugha ya Kihaya hususan lahaja ya Kihamba. Matokeo ya makala hii yanaonesha kuwa kiarudhi hiki hujitokeza katika nomino za lugha ya Kihaya hususan lahaja ya Kihamba. Baadhi ya nomino zilizochunguzwa katika makala hii ni pamoja na: *ékyáí*, *èkyàì*, *éndá*, *èndà*, *énkází*, *ènkàzì*, *mwízí*, *mwìzì*, *Rúhángá* na *rùhàngà*. Halikadhalika, toni C na J hujitokeza katika vitenzi vya lugha hii. Mathalani vitenzi vifuatavyo vimeonekana kupokea toni hizo. *kúsíngá*, *kùsìngà*, *kúúná*, *kùùnà*, *nááńdíká*, *nààǹdìkà*, *náchwá*, *nàchwà*, *nágéndá*, *nàgèndà*, *náyómbéká*, *nàyòmbèkà*, *názálá* na *nàzàlà*. Vilevile imebainika kuwa toni zina uamilifu wa kubadili maana ya maneno kwa mfano, *éká*→beba mgongoni, *èkà*→familia, *chúmbá*→pika, *chùmbà*[6]→chumba na kadhalika. Matokeo ya makala hii yanathibitisha pia kuwa toni hubadili kategoria za maneno

[6] Ni kisawe cha ekiyumba ambalo ni neno halisi la Kihaya. Neno chumba katika Kihaya limetokana na utohozi wa neno la Kiswahili chumba.

katika Kihamba, mathalani, nomino kuwa kitenzi au kitenzi kuwa nomino. Kwa mfano, *éká*→T, *èkà*→N, *chúmbá*→T, *chùmbà*→N, yáyá→T, yàyà→N na kadhalika. Makala hii imetoa ufafanuzi na kuonesha uamilifu wa toni katika lugha ya Kihaya hususan lahaja ya Kihamba. Hii imeonesha kuwa toni hujitokeza katika nomino na vitenzi vya Kihamba. Hivyo, imesaidia kutoa mwanga kwa wanaisimu juu ya kiarudhi hiki cha kifonolojia yaani toni sambamba na uamilifu wake. Inapendekezwa; lichunguzwe suala la ujitokezaji wa toni katika lahaja nyinginezo za lugha ya Kihaya; Kinyaihangiro, Kinyambo na Kiziba. Aidha, zichunguzwe toni katika lugha hii kwa kujikita katika aina nyingine za maneno tofauti na nomino na vitenzi. Kwa mfano, vielezi, vivumishi, vihisishi na kadhalika. Sambamba na hilo, tafiti fuatizi zifanyike kuhusiana na matumizi ya toni katika lugha nyingine tofauti na lugha ya Kihaya. Viarudhi vingine pia kama vile lafudhi, mkazo, nguvumsikiko, silabi, kiimbo, unguvunguvu, kidatu na wakaa vifanyiwe uchunguzi katika Kihaya na lugha nyingine duniani. Makala hii inachangia maarifa kuhusiana na kiarudhi cha toni katika lugha.

## Marejeleo

Bird, S. (1999). “Strategies for Representing Tone in African Writing Systems”. Katika *Written Language and Literacy*. (2), 1-44.

Buberwa, A. (2015). “Mofolojia ya Majina ya Mahali ya Kiswahili na Kihaya katika Jamii ya Wahaya”. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Byarushengo, E. R. (1975). “An Examination of the Segmental Phonology of Haya”. Tasnifu ya Umahiri. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Byarushengo, E. R. (1977). *Haya Grammatical Structure*, *Phonology*, *Grammar*, *Discourse*. Southern California Occasional Papers in Linguistics (6), June 1977. Published by The Department of Linguistics University of Southern California Los Angeles.

Byarushengo, E. R. na wenzake. (1976). *Tone, Accent, and Assertion in Haya*. Katika *Larry M. Hyman* (ed.) *Studies in Bantu Tonology*. Southern California Occasional Papers in Linguistics. (3), 183-206.

Carter, H. (1973). “Tonal data in Comparative Bantu”. Katika *African Language Studies*, (14), 36-52.

Downing, L. J. (2013). “Issues in the Phonology-Syntax Interface in African Languages”. Katika Orie, O. O. na Sanders, K. W. (wah.) *Selected Proceedings of the 43rd Annual Conference on African Linguistics*. 26-38. Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project.

France, B. & Kahigi, K. K. (2021). “Ulinganishi wa Michakato ya Kifonolojia katika Kinyambo na Kiswahili”. Katika *Jarida la CHALUFAKITA*. (3), 133-155.

Goldsmith, J. (1976). “An overview of Autosegmental Phonology”. Indiana University Linguistics Club, Bloomington.

Goldsmith, J. (1984). “Tone and Accent in Tonga”. Katika Clements, G. N na J. Goldsmith, (1984). *Autosegmental Studies in Bantu Tone*. Foris Publications. 281-339.

Hyman, L. M. & Byarushengo, E. R. (1984). “A Model of Haya Tonology”. Katika *Clements G. N na J. Goldsmith*. *Auto Segmental Studies in Bantu Tone*. Foris Publications. 53-103.

Leben, W. R. (1978). *The Representation of Tone*. Katika *Fromkin*, V. A (1978). *Tone*: *A Linguistic Survey*. 177-217, New York, Academic Press, INC. 103.

Kihore, Y. M. na wenzake. (2008). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo*. Chapa ya Nne. TUKI.

Kindole, E. (2012). “Toni katika Vitenzi vya Kihehe”. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kisseberth, C. W. (1984). *Digo Tonology*. Katika Clements, G. N na Goldsmith J. *Auto Segmental Studies in Bantu Tone*. 105-185, Dordrecht-Holland: Foris Publications.
Kisseberth, C. W. na David O. (2003). "Tone in Nurse and Philippson". Katika *The Bantu Languages*. 59-70.
Maho, J. F. (1999). *A Comparative Study of Bantu Noun Classes*. Goteborg, Orientalia Et Africana Gothoburgensia: Acta University Gothoburgensia.
Guthrie, Malcolm. (1971). *Comparative in BantuLanguages*. Vol. 2. Gregg International Publishers.
Massamba, D. P. B. (2011). *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia*. TATAKI.
Massamba, D. P. B. (2016). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. TUKI.
Mramba, P. (2020). "Ruwaza za Toni katika Vitenzi Visoukomo Changamani vya Kirombo". Katika *East African Journal of Swahili Studies,* 2(2), 168-196. https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.242.
Muzale, H. R. T. (2006). *Ikaningambo ya Oruhaya.* Language of Tanzania Project.
Odden, D. (2005). *Introduction Phonology*. Cambridge University Press.
Pike, K. (1948). *Tone Languages*. University of Michigan Press.